

## 10-Isti'aadhah Na Basmalah - Kuomba Kinga Na Kuanza Kwa Jina La Allaah

الإِسْتِعاذَةُ وَالبِسْمَلَةُ

Ni vyema ieleweke kuwa inapasa kwa kila mwenye kutaka kuanza kusoma Qur-aan kuleta Isti'aadhah kusema: "*A'uwduhu bil-LLaahi minash-shaytwaanir-rajiym*" yenye maana kuwa: "Najikinga kwa Allaah dhidi ya shaytwaan aliyefukuzwa", iwe mwanzo wa Suwrah, au katikati ya Suwrah kutokana na amri ya Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴾

**((Unapotaka kusoma Qur-aan basi (anza kwa) omba kinga kwa Allaah dhidi ya shaytwaan aliyefukuzwa (kuwekwa mbali na Rehema ya Allaah kwa kusema: *A'uwduhu biLLaahi minash-shaytwwanir-rajiym*))<sup>1</sup>**

Msomaji Qur-aan hutakiwa aisome Isti'aadhah *sirran* (kwa siri - kutotoa sauti); ikiwa anasoma kisomo chake bila ya kutoa sauti. Pia hutakiwa aisome kwa siri ikiwa anasoma hali ya kuwa yu peke yake iwe anasoma *jahran* (kwa sauti) au kwa siri (bila ya kutoa sauti). Ama ikiwa anasoma Qur-aan kwa kutoa sauti mbele ya hadhara ya watu wenye kumsikiliza atatakiwa aidhihirishe Isti'aadhah kwa kutoa sauti. Hali kadhaalika ikiwa kikundi cha watu wanaisoma Quraan mmoja baada ya mmoja kila mtu kusubiri zamu yake<sup>2</sup>, basi hutakikana msomaji wa kwanza kuisoma Isti'aadhah kwa kutoa sauti na waliobakia kuisoma *sirran* kila inapowadia zamu zao.

Wakati wo wote ule msomaji wa Qur-aan akitokezewa na jambo lolote lile la kupita lenye kumpelekea asite kusoma kisomo chake cha Qur-aan kama kwenda chafya, kukohoa, kupenga mafua au kueleza maneno yenye kuhusiana na kisomo chake mfano anapofasiri Qur-aan katika kikao cha darsa hicho hicho, huwa hatakiwi kuisoma tena Isti'aadhah.

Ama ikiwa jambo lililomtokezea ni katika mambo yasiyohusiana na Qur-aan, akashughulishwa mbali na Qur-aan, liwe la kuzungumza na mwenzake

---

<sup>1</sup> An-Nahl (16: 98)

<sup>2</sup>Ifahamike kwamba kukusanyika kusoma Qur-aan au du'aa kwa pamoja na sauti moja haipasi kabisa kwani hivyo ni uzushi. Hapo imekusudiwa ni kupeana zamu kila mtu anasoma kipekee akimaliza husoma mwengine mwenye zamu yake.

au kumjibu muulizaji, au kula au kunywa na kadhalika; basi ni vyema kuisoma tena Isti'aadhah atapotaka kuendelea na kisomo chake.

Asili ya utaratibu wa Isti'aadhah ni ile iliyokuja katika agizo la Allaah (سبحانه) <sup>3</sup> pale alipowaagiza wenye kutaka kusoma Qur-aan. Pia imethibiti nyongeza juu ya agizo la Allaah (سبحانه وتعالى) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه) <sup>4</sup>; hivyo inaruhusiwa kwa msomaji kuileta hiyo nyongeza kwa kuwa ni kamfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwa hivyo, msomaji ana uhuru wa kuchaguwa kati ya matamshi haya:

- أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

- أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

### Tanbih:

Hapatakiwi kusomwa Isti'aadhah baada ya mtu kusema "Allaah Anasema:", kwani huenda ikafahamika kwa Allaah Anajikinga kwa shaytwaan, na hii ni katika makosa yaliyo mabaya ambayo wengi hutumbukia. Ikibidi kuanza na "Allaah Anasema" basi sema: "Allaah Anasema; **baada ya A'udhubiLaahi minash-shaytwaanir-Rajiyim**".

<sup>3</sup>Aayah iliyotangulia ya An-Nahl (16: 98)

<sup>4</sup>Kutoka kwa Abu Sa'iyd al-Khudriy kwamba: "Alikuwa Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) anaposimama usiku akifunguwa Swalaah yake husema:

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ وَتَبَارَكَ اسْمُكَ وَتَعَالَى جَدُّكَ وَلَا إِلَهَ غَيْرُكَ

((Kutakasika ni Kwako, Ee Allaah, na Sifa njema ni Zako, na limetukuka Jina Lako, na Utukufu ni Wako, na hapana ilaah [mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki], asiyekuwa Wewe)), kisha huleta takbiyra ((اللَّهُ أَكْبَرُ)) kisha husoma:

أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

((Najikinga kwa Allaah As-Samiy'ul-'Aliym (Mwenye kusikia yote daima, Mjuzi wa yote daima) kutokana na Shaytwaan aliufukuzwa)) Imepokelewa na at-Tirmidhiy, katika mlango wa anayoyasema katika kufunguwa Swalaah, Hadiyth 242.